BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tatu – Tarehe 8 Februari, 2019.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2018/2019.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

38. MHESHIMIWA TATU MOHAMED USSI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

    Kwa kuwa Idara ya Mazingira inafanya kazi kubwa ya kuhamasisha wananchi katika kuyatunza mazingira katika kijiji cha Jaalani kilichopo Wilaya ya Mkoani Shehia ya Ng'ombeni, ambacho kimeathirika sana kimazingira na kusababisha maji ya chumvi kupanda kwa kasi.
    (a) Je, Wizara inalijua hilo.

(b) Je, Idara ya Mazingira inalishughulikia vipi suala la mmong'onyoko wa ardhi uliopo katika Shehia ya Ng'ombeni ambalo linaathiriwa kwa kupanda kwa maji ya chumvi katika eneo hilo.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

62. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mkoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kituo cha Afya cha Fuoni kinatoa huduma ya kujifungua kwa masaa 24 kwa siku. Hivyo gharama za umeme huongezeka na kwa kuwa fedha za umeme wanazopatiwa hazitoshelezi mahitaji.

Je, Wizara ina mpango gani wa kuwaongezea fedha za umeme ili wapate kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

143. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

Kampuni ya ulinzi ni biashara iliyoshika kasi hapa nchini kwetu na kuzalisha ajira nyingi. Hata hivyo, kuna taarifa kwamba makampuni mengi yanayofanyakazi hapa nchini hayajasajiliwa na mengine yamesajiliwa nje ya nchi na wafanyakazi wao hutoka nje ya Zanzibar.

Je, ni makampuni mangapi ya ulinzi yanafanya kazi Zanzibar na ngapi yamesajiliwa.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

47. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya 2015, Kifungu cha 12(1)(a)(b) kinaipa mamlaka Tume ya Maadili ya viongozi wa Umma kuchunguza malalamiko ya Viongozi wa Umma wanaokiuka maadili.

(a) Je, kwa kipindi cha 2015 - 2018 ni viongozi wangapi waliolalamikiwa kukiuka kwa kutumia vibaya mamlaka yao kwa maslahi binafsi.

(b) Je, ni taasisi gani ambazo baadhi ya viongozi wake walilalamikiwa na hatua ambazo zilichukuliwa na utekelezaji ulikuwaje.

(c) Je, viongozi wa umma wangapi ambao walifukuzwa kazi ama kushtakiwa au kufungwa baada ya kutiwa hatiani kwa matumizi mabaya ya mali ya umma au matumizi mabaya ya madaraka yao.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

21. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Serikali kwa nia njema imewapa fursa wafanyabiashara kufanya biashara huru lakini suala la mfumuko wa bei bado ni tatizo. Kila mfanyabiashara huamua kuweka bei yake na kufanya maisha ya wananchi kuwa magumu.

(a) Je, Serikali inalijua hilo.

(b) Je, Serikali imefanya utafiti na kuangalia kuwa maisha yanakuwa magumu kutokana na mfumo gani.

(c) Je, Serikali haioni kuwaachia wafanyabiashara kujiamulia bei wanavyotaka ni kuwaongezea wananchi ugumu wa maisha.

Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale:

139. MHESHIMIWA ALI SULEIMAN ALI (Jimbo la Kijitoupele) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale.

Nalipongeza Shirika la Habari la Zanzibar ZBC chini ya Mkurugenzi wake na watendaji wake wote kwa kuendeleza mashindano ya kombe la Yamle Yamle CUP. Mashindano hayo ni mazuri na wanamichezo hutoka sehemu mbali mbali kushuhudia timu zao.

Je, Wizara ina mpango gani ili kuyakuza mashindano hayo.

Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali:

140. MHESHIMIWA PANYA ALI ABDALLA (Nafasi za Wanawake) -Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kuna malalamiko ya walimu wanaotoka mjini kwenda kufundisha vijijini kuchelewa kupata nauli zao na kuathiri utendaji wa kazi zao.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kutatua tatizo hili.

(b) Je, kucheleweshe kutoa nauli kwa walimu, hatuoni kuwa kunasababisha matokeo mabaya kwa wanafunzi kutokana na walimu kupanda magari ya kudandia, magari ya mchanga na kuchelewa kufika kazini.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

7. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Hapo zamani nyumba za ghorofa zilikuwa ni ghorofa moja kama imezidi ni mbili, hivyo yanapotokea matatizo ilikuwa rahisi kuokoa waliomo ndani. Lakini hivi sasa tumeanza kujenga majengo marefu hadi kufikia ghorofa 10 na kuendelea.

(a) Je, vifaa tunavyovitumia vinakidhi ujenzi wa ghorofa kubwa.

(b) Je, mazingira ya ardhi yetu ina uwezo wa kuhimili mpaka ghorofa ngapi.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

12. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Katika jitihada za Serikali kuendeleza kilimo cha kisasa na kutokomeza njaa hivi karibuni yalifunguliwa maonesho ya kilimo ya Siku ya Chakula Duniani hapo Chamanangwe, Ole Mkoa wa Kaskazini Pemba. Maonyesho hayo yalionesha maendeleo ya kilimo, mifugo na biashara za kila aina, lakini bado wananchi hawajaelewa hasa nini madhumuni ya jambo lile la kihistoria na mfano kwa nchi nyengine.

(a) Je, nini madhumuni ya kutengenezwa eneo lile.

(b) Je, eneo lile litaendelea kutumika kwa mpango gani.

(c) Je, eneo lile litajiendesha kibiashara au kihuduma zaidi.

.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

48. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa kuwa Serikali hutumia fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara zetu za Unguja na Pemba. Kwa kuwa zipo barabara ambazo zimeshafanya athari ya kuchimbuka mashimo kama vile barabara ya Konde/Wete eneo la Kizimbani na chini ya “cross” ya Kuungoni na barabara ya Gando ambazo zilijengwa na Kampuni ya Mecco.

(a) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa za kuzihami barabara hizo ili zisiendelee kuchimbuka na kupelekea kupata hasara kubwa zaidi.

(b) Je, kuna utaratibu gari wa kuyakagua malori ya mizigo ili yasibebe mizigo yenye uzito mkubwa zaidi ya uwezo wa barabara hizo ili kudhibiti uharibifu wa barabara zetu.

(c) Je, kuna utaratibu gani wa kuweka vibao ‘sign board’ vya barabara vinavyoonyesha uzito wa malori ya mizigo yatakayoruhusiwa kupita kwenye barabara hizo.

III. HOJA ZA KAMATI:

Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:

Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2018/2019.

Zanzibar,
8 Februari, 2019.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.